



**GAZETI RASMI LA SERIKALI YA
MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVI Nam. 6675

13 Novemba, 2017

Bei Shs. 15,000/=

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

Hutolewa kila Ijumaa

YALIYOMO

Ukurasa

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya 2004 na Kutunga Sheria mpya ya Mwenendo wa Jinai na Kuweka utaratibu Bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikilizaji wa Kesi za Jinai na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. 231

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada uliyotajwa hapo chini umetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Mswada wa Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai na Kutunga Sheria mpya Mwenendo wa Jinai

TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi ulioanza tarehe 27 Septemba, 2017 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
13 Novemba, 2017

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na
Katibu Mkuu Kiongozi.***

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA**WA**

**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MWENENDO WA JINAI
NAM. 7 YA 2004 NA KUTUNGA SHERIA MPYA MWENENDO
WA JINAI NA KUWEKA UTARATIBU BORA WA UPELELEZI
WA MAKOSA YA JINAI NA USIKILIZAJI WA KESI ZA JINAI NA
MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.**

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi.

**SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI**

- Jina fupi na kuanza kutumika **1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mwenendo wa Jinai, 2018 na itaanza kutumika baada ya kuwekwa saini na Rais.
- Ufafanuzi **2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

“kosa lenye dhamana” maana yake ni kosa ambalo mshtakiwa anaweza kupewa dhamana na Mahakama yoyote au mkuu wa kituo cha polisi kama ilivyoelezwa chini ya kifungu 151(1);

“kosa analoweza kukamatwa mtu bila ya hati” maana yake ni kosa ambalo afisa wa polisi anaweza, kwa mujibu wa Jadwali ya Kwanza la Sheria hii au chini ya sheria yoyote ambayo kwa wakati huo inatumika, kukamata bila ya hati;

“mtoto” maana yake ni mtu aliye chini ya umri wa miaka 18;

“malalamiko” maana yake ni tuhuma zilizotolewa kwa mdomo au kwa maandishi mbele ya hakimu kwa lengo la kuchukua hatua chini ya Sheria hii;

“mlalamikaji” katika uendeshaji mashtaka binafsi maana yake ni mwendesha mashtaka binafsi au mtu anayepeleka malalamiko mbele ya Mahkama, katika mashtaka yote ya umma maana yake mtu anayewasilisha kesi mbele ya Mahakama kwa niaba ya Serikali;

“Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai” maana yake ni mtu mwenye dhamana ya kuendesha mashtaka ya jinai aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar, 1984 na pale inapofaa itajumuisha wakili wa Serikali, mwendesha mashtaka wa umma au mtu mwengine yeyote anayeendesha mashtaka chini ya maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

“upelelezi” unajumuisha nyenendo zote chini ya Sheria hii kwa ajili ya ukusanyaji wa ushahidi zinazofanywa na afisa wa polisi au na mtu mwengine yeyote, asiyekuwa hakimu, ambaye amepewa